# Ayubu



Published by the Comic Bible Society, LLC
Copyright © 2021

Kingstone Comics maintains copyright to this comic book as provided by United States copyright law.

Print and digital copies of this version may be freely distributed without penalty under a Creative Commons license.


NCHI YA USI
NYUMBANI MWA AYUB NA FAMILIA YAKE.
AYUB, BABA MWENYE WATOTO SABA WA KIUME NA WATATU WA KIKE, ALIYEJULIKANA KOTE UPANDE WA MASHARIKI SIO TU KWA MALI YAKE--
--ILA KWA KUMCHA MUNGU NA KUJITOLEA KWA FAMILIA, MARAFIKI NA WATU WENZAKE.
NAINUA KIKOMBE CHANGU KWA MWENYEJI WETU!
AYUB! MTU NINAYELENGA KUWA KAMA ALIVYO NA MTU NINAYETUMAINI WATOTO WANGU WATALENGA KUWA KAMA ALIVYO!
ELIFAZI RAFIKI YANGU TANGU JADI! U MWEMA!
NI MWEMA? TAZAMA SHEREHE ULIYOTUANDALIA!
AAH, U RAFIKI YANGU.
LA, ZAIDI, WEWE NI KAMA FAMILIA!
MARAFIKI WAKE WA KARIBU WALITOKA SEHEMU ZETU ZA ENEO HILO...


WASEMA "FAMILIA"! NATAMANI INGELIKUA HIVYO!
MAANAKE HAKUNA ANAYEPENDA FAMILIA YAKE KAMA WEWE AYUB!
ELIFAZI, MTEMANI KUTOKA UTEMANI, MAHALI PALIPOJULIKANA KWA HEKIMA YAKE.
NDIO, MTU ANAYEIPENDA FAMILIA YAKE LAKINI PIA ANAYEPENDA HEKIMA!
BILDADI. MSHUHI, MJUKUU WA SHUAH, MWANA WA IBRAHIMU, KUTOKA JANGWA LA KIARABU KWENYE NCHI YA MASHARIKI.
AYUB! SIJUI ULICHOKIFANYA KUSTAHILI MALI HII NA FAMILIA--
LAKINI NIAMBIE ILI MIMI PIA NIFANYE!
SOFARI. MNAAMATHI, KUTOKA JIJI LA NAAMAH MPAKANI.
ALIKUWA MKARIMU NA MUAMINIFU KWA AYUB, NA MCHA MUNGU!
NI KITU KIZURI NI MNYENYEKEVU, AMA HIZI SIFA ZOTE ZINGEMFURISHA KICHWA!
ELIHU, MBUSI. KIJANA KWA MARAFIKI WA AYUB WA KARIBU JINA LAKE LINA MAANA "MUNGU WANGU NDIYE."


BABA?
NAONDOKA SASA. OMAR AMEANDAA SHEREHE NYENGINE.
NAFURAHI KUWA WANANGU BADO WANAFURAHIA KUWA PAMOJA!
WAONDOKA TAYARI?
KUMBUKA KUWA NA USTAARABU! WAKUMBUSHE KAKA ZAKO NA DADA ZAKO--
SAWA BABA!
NIMEMUAMBIA SETHI AKUPELE. ATABAKI HAPO AKULETE NYUMBANI ASUBUHI.
WAPE WOTE SALAMU ZETU!
TWASHKURU KWA YOTE UNAYOTUFANYIA-SANA SANA KAFARA-- NA HATUTAFANYA LOLOTE KUKUAIBISHA! HATA MUNGU! NINAAHIDI!

AYUB 1:4


KAFARA?
AYUB ANATOA KAFARA KWA AJILI YA WATOTO WETU IWAPO WATATENDA DHAMBI WANAPOSHEREHEKEA.
MUNGU ANAULIZIA MALIPO KWA DHAMBI ZETU. HATUKO WATAKATIFU WALA WASAFI.
NAWAPENDA, KWA HIYO NAENDA KWA BWANA KWA NIABA YAO.
UTAFANYA HIVYO WAKATI GANI?
WANASHEREHEKEA HADI USIKU WA MANANE, KWA HIVYO SITATOA KAFARA HADI ASUBUHI.
USIJALI, SITAKATIZA SHEREHE YETU KATIKATI!
AAH, NILITAKA HIVYO TU!
KAMA KUNA MTU AWEZAYE KUTOA KAFARA KWA NIABA YA WENZAKE NI WEWE AYUB.
HAPANA, ELIHU. USIPIME MTU HIVYO --
--WAKATI MIE SI MKUU ZAIDI KUMLIKO YEYOTE HAPA.
SIO MBELE YA MUNGU, MBELE YA UTAKATIFU WAKE SOTE TU WENYE DHAMBI NA WACHAFU...
SASA TULE CHAKULA CHAPOA!


MAPEMA SIKU ILIYOFUATA.
AYUB ALITENDA ALIVYONENA.
KAMA KAWAIDA YAKE.
NAJA KWAKO, BWANA WANGU, KWA NIABA YA WANANGU.
UMENIBARIKI NAO--
--KAMA WAMEKULAANI MIOYONI MWAO IKUBALI KAFARA HII!
AYUB ALIJUA MUNGU ALIYAANGALIA MATENDO YAKE.
LAKINI HAKUWA NA HABARI MWENGINE--


MBINGUNI, WANA WA MUNGU WALIJILETA MBELE YAKE.
NA MWENGINE -- MTAZAMAJI ASIYEONEKA-NA--AKAJA KATI YAO PIA.
ALIYEANGUKA.
ALIYETANGULIA KUANGUKA.
IBILISI.


UMETOKA WAPI?
NIMEKUWA KATI YA WATU WA DUNIA.
NIKIENDA MBELE NA NYUMA, NIKIWATAZAMA VIUMBE UNAOWAPENDA ZAIDI.
NDIO, UMEFANYA HIVYO.


JE, UMEMUONA MTUMISHI WANGU AYUB?
NAAM.
HAKUNA KAMA YEYE DUNIANI. ANIOGOPA. ACHUKIA UOVU. APENDA UTAKATIFU.
AH, NDIO.
MBONA ASIKUOGOPE?
WAMLINDA! WAMBARIKI!
ANA MAKAO YA AJABU, WINGI WA MIFUGO, NA FAMILIA KUBWA YENYE AFYA!
LAKINI...
MUONDOLEE NA ATAKULAANI.
NIACHE NICHUKUE BARAKA ZAKE ZOTE. UONE.
NAKUPA RUHUSA KUCHUKUA ALICHO NACHO ILA USIMGUSE.
SITAUGUSA MWILI WAKE...
KWA HIYO MSHTAKI AKAONDOKA KWENYE UWEPO WA BWANA.



AYUB 1:8-12


SHAMBANI MWA AYUB.
NJOO BI KIZEE...
NINI HIYO?
THUMP THUMP
KIMBIA!!!


KWENYE MILIMA MWISHO WA SHAMBA LA AYUB, WALIKOLISHA MIFUGO YAKE.
HIYO NI HARUFU YA NINI?
KILA MTU!
KIMBIA!
KUNA...



AYUB 1:16


MSAFARA WA NGAMIA ZA AYUB.
WASKIA?
YATOKA UPANDE ULE, LAKINI NI NINI?
WAKALDAYO!
NI UVAMIZI!
WAKO KILA MAHALI!
TUMEZINGIRWA!


NYUMBA YA MWANA WA KWANZA, OMAR.
ULILALA VIZURI COL?
NDIO LAKINI HAPANA KWA SABABU YENU, DAVINIA!
JETHI ALIKICHEZA KINANDA CHAKE KWA MDA GANI NILIPOENDA KULALA?
MDA MREFU COL! MREFU SANA!
TUTAFUTE CHAKULA.
MUME WANGU BADO AMELALA, LAKINI SAA ZOTE AKIAMKA ANA NJAA.
KUNA KINGI KILICHOBAKI! OMAR NA VIJANA WENGINE BADO WAKO MACHO!
WASKIA KITU?
SIJAWAHI KUONA...
INA...INAKUJA HAPA TULIPO!!!
TUONDOKENI HAPA!
TUTAENDA WAPI?




AYUB 1:19


ASANTE KWA KUJUMUIKA NAMI!
TUTAONANA HIVI KARIBUNI!
AYUB NILIKUONA LEO ASUBUHI UKITOA KAFARA YAKO.
UNAVYOMCHA MUNGU HAUNA MWENZAKO.
NI MFANO NINAOUTHAMINI MOYONI.
ASANTE, ELIHU.
NI MFANO NINAOUTHAMINI MOYONI, PIA.
WANIPAKA MAFUTA, MKE WANGU!
KUKUPAKA MAFUTA? SIWEZI!
SASA NAWEZA KUPATA ILE SINIA YA DHAHABU ANAYOIUZA FUNDI CHUMA PALE MJINI?
LABDA...BAADA YA KUNIPAKA MAFUTA ZAIDI!
BWANA! BWANA!


EBEDI, NINI KIMEKUFANYIKIA?
BWANA... MIMI PEKEE NDIYE NIMEJISALIMISHA...
WASEBA...WALIVAMIA BILA TAHADHARI NA KUUA KILA MTU NA KUCHUKUA KILA KITU!
HANNAM, MLIVAMIWA PIA?
LA...MOTO MKUU ULITOKA MBINGUNI!
ULICHOMA MASHAMBA NA KONDOO NA WACHUNGAJI ILA MIMI!
HAIWEZEKANI!
TARUM? TAFADHALI NIAMBIE WALETA HABARI NJEMA!
TUMEVAMIWA NA WAKALDAYO!
WALITUZINGIRA NA KUUA KILA MTU NA WAKAWACHUKUA NGAMIA WOTE!
BWANA! JAMBO BAYA LIMETENDEKA!
NAJUA! NIMESIKIA!
WATUMISHI WAMEKUFA! MIFUGO IMEUWAWA NA KUIBWA! YASIKITISHA!
HAPANA BWANA! KITU KIBAYA ZAIDI!
ZAIDI!?! NI NINI KINAWEZA KUWA KIBAYA ZAIDI, SETHI?



WATOTO WAKO WA KIKE NA WA KIUME WOTE WALIKUWA KWA MWANAO WA KWANZA WAKISHEREHEKEA...
NAJUA HAYA! UMEKUJA KUTUAMBIA NINI?
UPEPO MKUU ULIKUJA BWANA...ULIIPIGA NYUMBA...
ILIANGUKA... TULIANGALIA KWENYE MAPOROMOKO TUKAPATA KILA MTU, LAKINI WALIKUWA WOTE...WOTE
HAPANA. JAMANI HAPANA... HAPANA...
HAPANA!!! HAIWEZEKANI!!!
HAPANA!!!
VITOTO VYANGU... WATOTO WANGU WAPENZI...




AYUB 1:18-19



AYUB 1:20


HAPANA!
HAPANA!
HAPANA!


SIKU CHACHE BAADAYE...


NILITOKA TUMBONI MWA MAMANGU NILI UCHI!
NA NITARUDI UCHI KABURINI MWA ARDHI!
BWANA ALINIPA VINGI SANA!
NA SASA AMEVICHUKUA VYOTE!!!
BWANA, JINA LAKO LITUKUZWE!
SIJUI KWA NINI ULIRUHUSU HAYA YAFANYIKE!
NINALOWEZA KUFANYA SASA NI KUOMBA NGUVU NA FARAJA YAKO...
IZIBE!



AYUB 1:21-22


TENA, IKAFIKA SIKU WANA WA MUNGU WALIPOJIPELEKA MBELE YA BWANA.
NA TENA, WA KWANZA KATI YA WALIOANGUKA AKAJA KATI YAO PIA.
NILIKUAMBIA HAKUNA KAMA MTUMISHI WANGU, AYUB.
ULIJARIBU KUMGEUZA DHIDI YANGU, ILA AMEBAKI BILA LAWAMA.
BILA SHAKA, KWA SABABU MOJA TU!
SIKURUHUSIWA KUMGUSA.
MAISHA YAKE JE? BINAADAMU ATATOA KILA KITU KWA AJILI YA UHAI WAKE!
ANGEKULAANI KAMA MWILI NA MIFUPA YAKE INGEGUSWA NA KUTESWA!
NITARUHUSU.
WADHANI WAJUA MATOKEO.
NINAJUA, NA NINAELEWA KIWANGO GANI.
AKO MIKONONI MWAKO
FANYA UTAKAVYO, BORA HATIMAYE AISHI.
"KIWANGO GANI" KWA HAKIKA.


AYUB, WAFANYA NINI?
NGOZI YANGU YAWASHA...SIJAWAHI KUHISI NAMNA HII...
RUDI ULALE TU!
AHHHH... NAUMWA
AYUB? KUNA NINI?
AYUB?
*AH... HAPANA...*



AYUB 2:7


NAUMWA... KILA MAHALI...
NGOZI YANGU... TUMBO LANGU... KICHWA CHANGU... KUPUMUA...
JIANGALIE!!!
BADO WASEMA, "LIBARIKIWE JINA LA MUNGU?"
ARRRH!!!
RRRAAUGH!!!
KRAK
FANYA IACHE... FANYA IACHE...
AYUB!
MLAANI MUNGU TU!

AYUB 2:8-9


MLAANI UFE!!!
TUTAKUBALI MAZURI TOKA KWA MUNGU, TULIVYOFANYA MIONGO ILIYOPITA, WALA SIO MABAYA?
NATARAJIA MAZUNGUMZO YA KIPUMBAVU TOKA KWA WENGINE ILA SIO TOKA KWAKO!
NA SASA NAMPOTEZA, PIA...




YOTE... KAPOTEA...
MIFUGO YANGU... WATUMISHI WANGU... WANANGU...
VUMBI NA JIVU...


YULE PALE!!!
PALE!!!
UNA UHAKIKA? YULE NI...HAKAI KAMA MWANADAMU!
AYUB, TULIKUJA PUNDE TU TULIVYOSIKIA!
KWANZA WAPOTEZA KILA KITU, WAKIWAMO WANAO!
SASA HAYA!!!
AH AYUB... POLE SANA!!!
TUATASONONEKA NAWE KAMA ILIVYO DESTURI.
ASANTENI... MARAFIKI ZANGU...


MARAFIKI ZAKE WALIKAA KIMYA NAYE KWA SIKU SABA--
--MCHANA NA USIKU.
MPAKA, HATIMAYE...
ILAANIWE SIKU NILIYOZALIWA!!!



AYUB 2:11-3:1




AYUB 3-4:11, 6:11


UOVU NA SHIDA!!!
UMEFANYA KITU KUSTAHILI HAYA!
USIKU MMOJA NILIKOSA USINGIZI, NIKAONA KWENYE NDOTO...
ROHO ALIPITA JUU YANGU NA AKISIMAMA MBELE YANGU AKASEMA:
WANADAMU WANAWEZA KUWA WATAKATIFU MBELE YA MUNGU?
JE BINADAMU, KIUMBE, AWEZA KUWA MTAKATIFU MBELE YA MUNGU, MUUMBA?
KAMA MALAIKA WAWEZA KUANGUKA JE WANAADAMU WAJENGAO NYUMBA ZINAZOGEUKA KUWA VUMBI NA WA WANA MILI INAYOVUNJIKA KAMA NONDO!
HUU NI USHAURI WANGU, AYUB, KUTOKA MIAKA YA UZOEFU NA UANGALIFU.
MTAFUTE MUNGU!
NA UFURAHI MUNGU AMECHAGUA KUKUREKEBISHA!
NIFURAHI? JUU YA HAYA?
AFANYA HIVI KUKUSAIDIA! AWEZA KUKUUMIZA LAKINI AKIFINIKA KIDONDA!
TUBU DHAMBI YAKO MBAYA NA UTAKUWA MZIMA!
ELIFAZI NAWEZA KUSEMA KITU?


WANANGU WALALA MAUTINI NA MWILI WANGU UMEJAWA NA UGONJWA!
LAKINI SIJAWAHI KUMSHUKU MUNGU NA KUKATAA MANENO YAKE!
NIONYESHE NILICHOKOSEA KUSTAHILI HAYA, NA NITAWACHA!
HUWEZI, SIO?
NIANGALIE USONI ELIFAZI!
TAZAMA KAMA NADANGANYA NISEMAPO SINA HATIA!
AH MUNGU! MWILI WANGU UMEPALWA DAMU NA TOPE NA MINYOO NA USAHA!
NALIA KWA UCHUNGU NA MAUMIVU! WAONA UCHUNGU ROHONI MWANGU!
NIMETENDA DHAMBI ANAVYOSEMA ELIFAZI? NIONYESHE!
UTAKAPONIONYESHA TU, WAJUA NITATUBU!
KWA SASA NATAKA KULALA TU KWENYE ARDHI NIACHE MWILI WANGU UPOTELEE KWENYE VUMBI...
AYUB?


MANENO YAKO NI KAMA UPEPO UNAOVUMA!
MUNGU HAIPOTOSHI HAKI!
KAMA KWELI UNGELIKUWA MSAFI ANGEKUWA ASHAKUJIBU.
FIKIRIA HEKIMA YA MABABA ZETU... NA HEKIMA YA MABABU ZAO.
SIKU ZETU HAPA ULIMWENGUNI NI FUPI KWA HIYO LAZIMA TUJIFUNZE KUTOKA KWA HEKIMA YA MABABU.
FIKIRIA MMEA BILA MAJI. HIVYO NDIVYO ALIVYO MTU ALIYEMSAHAU MUNGU.
MIMEA ILIYOKUFA NA MAGUGU HUNG'OLEWA, MKULIMA HAFIKIRII MARA MBILI--
--ANAITUPA!
MUNGU HAWATUPI WASIO NA HATIA!
NA HAWAINUI WATENDA MAOVU!
TUBU AYUB, NA ATAKIJAZA KINYWA CHAKO NA KICHEKO!


BILDADI, HATA KAMA NINGEKUWA MTU MSAFI, MUADILIFU, MTAKATIFU ZAIDI YA WOTE BADO NINGEHITAJI KUOMBA REHEMA YAKE!
KWENDA MBELE YA ALIYE MTAKATIFU KAMA YEYE, NINGEHITAJI MPATANISHI MTAKATIFU AONGEE KWA NIABA YANGU!
LAKINI NANI? HAKUNA!
MUNGU, MIKONO YAKO ILINIUMBA, MBONA UNIANGAMIZE?
MBONA UACHE HATA MACHO YANGU YAONE MWANGA WA SIKU NILIPOZALIWA?
MBONA UKUBALIE GIZA HILI MAISHANI, WAKATI NINGEBAKIA TU GIZANI?
MANENO! MANENO! MANENO!
MANENO HAYALETI MSAMAHA NA UKOMBOZI!
WASEMA U MSAFI, WASEMA HUNA HATIA--LAKINI KUSEMA HAIMAANISHAI IKO HIVYO!
SISEMI HIVYO!
MUNGU AWAJUA WATU WALAGHAI, AYUB! ANAZINGATIA WATU WAOVU!
NA WATU WAPUMBAVU AMBAO HAWAWEZI KUWA NA HEKIMA VILE TU FARASI HAWEZI KUWA MWANADAMU!
WEWE NI YUPI, AYUB?
MTU MUOVU, MLAGHAI AU MPUMBAVU?

AYUB 9-11:12


TUBU, AYUB. TAYARISHA MOYO WAKO. TUPA UOVU NJE.
KISHA UTAWEZA KUWA NA IMANI NA USHUPAVU!
LAKINI IMANI YA MTU MUOVU INAKUWA PUMZI YA KUKATA ROHO!
WATU WATAPATA HEKIMA WAPI NYINYI WATATU MTAKAPOKUFA?
AYUB, HUU SI WAKATI WA DHIHAKA...
BAH! MWATEMA MANENO MACHACHE YA HEKIMA LAKINI YAMECHANGANYIKANA NA UPUMBAVU MNAONITAPIKIA!
ANGALIA ULIMWENGU, ELIFAZI!
SAA ZENGINE WATU WENYE HAKI NA WALIONYOOKA WANA NJAA, NA WEZI HUFANIKIWA!
BILDADI, WATU WAZEE WANA HEKIMA YA MIAKA MINGI NA YA MABABA ZAO, LAKINI HEKIMA YOTE HUTOKA KWA MUNGU!
SOFARI, WANISINGIZIA, KUJIDAI WAONGEA KWA NIABA YA MUNGU, LAKINI MANENO YAKO NI UONGO!
UONGO!
METHALI ZA MAJIVU! HOJA ZA UDONGO!
AYUB, TWAJARIBU KUKUSAIDIA!
BASI NYAMAZENI!
HAIJALISHI ANACHOKIFANYA MUNGU, NITAMUAMINI!
MAANAKE MUNGU NI MWENYE HAKI! NA MZURI! NA MTAKATIFU! NA UKOMBOZI WANGU!



AYUB 13:20-17:16


WADHANI TU WAPUMBAVU, AU?
TUNA MACHO, TWAWEZA KUONA USHAHIDI!
HAYA NDIO HUMFANYIKIA MTU MUOVU!
VITISHO VINAMZUNGUKA KISHA ATUPWA GIZANI!
WATU WANAMUONA NA KUSHIKWA NA HAMAKI KISHA ULIMWENGU WAMSAHAU!
WAELEWA?
NDIO! YAFANYIKA SASA HIVI!
NACHUKULIWA KAMA MGENI KWA NYUMBA YANGU MWENYEWE!
NIHURUMIE BILDADI!
SOFARI NA ELIFAZI, NILIWAZENI NA KUNIPA REHEMA!
ELIHU USINIACHE!
AH, KAMA TU MANENO YANGU YANGEDUMU, LAITI YANGEANDIKWA KWENYE KITABU KWA WALE WATAOKUJA BAADA YANGU...
NAJUA MTETEAJI WANGU YU HAI.
NA BAADA YA NGOZI YANGU NA MISULI NA MIFUPA YANGU KUHARIBIWA BADO NITAMUONA MUNGU!
LAKINI NYIE!!!



AYUB 18-19:27




AYUB 19:28-20:29


KAMA MTANISINGIZIA HIVI ANGALIENI MACHO YANGU YALIYOJAA MACHOZI NA USO WANGU ULIOJAA UCHUNGU!!
MWASEMA WAOVU WAFA WANGALI WACHANGA! SIO KWELI!
MVUA YAWANYESHEA WENYE HAKI NA WASO HAKI!
SIELEWI KWA NINI...MUNGU TU AJUAYE. HAKUNA ANAYEWEZA KUELEWA NJIA ZAKE!
MUNGU HAKUADHIBU KWA SABABU YA UTAKATIFU WAKO.
WATU WAOVU HUFICHA DHAMBI ZAO KUTOKA MACHO LAKINI HUWEZI KUJIFICHA TOKA KWA MUNGU!
LAKINI ELIFAZI, NIMESHINDA NIKITAKA KUUJUA MOYO WA MUNGU MAISHA YANGU.
ULIVYOSEMA, MUNGU AUJUA MOYO WANGU.
NAJUA AFADHALI NIISHI NA MANENO YANAYOTOKA KINYWANI MWAKE KULIKO MKATE...
SISKII HAYO MANENO HIVI SASA!


WATU HUIBA NA KUHARIBU. MASKINI WAKO NJAA NA UCHI.
MTU AMUUA MWENZAKE. WAUME NA WAKE WAZINI.
KWENYE FINIKO LA GIZA, WATU WA GIZA WAFANYA VITU VYA GIZANI.
KULINGANA NAO MI SIO MUOVU; KULINGANA NA MUNGU, LABDA.
NA NINGEUFUTILIA MBALI HUO UOVU KAMA NINGELUWA NA NGUVU ZA MUNGU.
LAKINI MUNGU HAFANYI. KWA NINI?
LABDA NAFAA NIFURAHIE MAANAKE HAFANYI HIVYO AU NINGEFUTILIWA MBALI PIA!
AYUB, WASKIZA UNACHOKISEMA?
NIMESEMA UONGO WOWOTE?
HAPANA. NI KWELI KUWA MUNGU ANA NGUVU NA YU MTAATIFU NA SAFI.
NA BINADAMU?
BINADAMU NI BUU, AYUB!
WEWE AYUB, U MNYOO MACHONI MWA MINGU...
AJABU, BILDADI!


UMEIRIDHISHA NAFSI YANGU!
NIAMBIE ULIKOPATA HEKIMA HII YOTE?
AYUB, NAKUONYESHA NILICHOJIFUNZA KUTOKA KWA WATU WENGINE WENYE HEKIMA!
AH. "WATU WENGINE WENYE HEKIMA." SAWA.
USO WA DUNIA, UNDANI WA BAHARI, UPANA WA MBINGU--
--MUNGU ALIVIUMBA VYOTE, NA NI KIONJO TU CHA ANACHOKIWEZA!
MUNGU AMECHUKUA KILA KITU ILA UCHUNGU ROHONI MWANGU.
ANAWEZA ASINIZUNGUMZIE LAKINI SITAONGEA VIBAYA KUMHUSU KAMA MLIVYOFANYA!
KILA NENO NINALOLITAMKA LANIUMIZA ...
NINA WAKATI WA UKWELI TU.
WAFALME WACHIMBA ARDHI, WATU WAUA KUIBA MALI, WATAKATIFU WAFANYIA MALI YAO...
WATAFUTA DHAHABU NA FEDHA, ZILIZOCHIMBWA TOKA ARDHINI.


DHAHABU NA FEDHA ZAWEZA KUNUNULIWA.
DHAHABU NA FEDHA ZAWEZA KUPATIKANA.
DHAHABU NA FEDHA ZAWEZA KUKUBALIKA.
LAKINI DHAHABU NA FEDHA NI HAZINA INAYOWEZA KUIBIWA!
HAZINA INAYOWEZA KUPOTEA!
HAZINA AMBAYO MWISHOWE ITAPOTEA.
LAKINI SIO HAZINA KUU ZAIDI...
NA HAZINA KUU ZAIDI NI NINI?
HEKIMA!
SIO TU UJUZI ULIOFUNZWA NA MABABU, MAPITIO AU KUONA!
NA HEKIMA YATOKA WAPI?
"KUMCHA MUNGU NI MWANZO WA HEKIMA; KUEPUKA UOVU NI MWANZO WA HEKIMA."
HEKIMA NI KUJARIBU KUYAELEWA MAISHA KAMA ATAKAVYO MUNGU!
NATAMANI SIKU ZA ZAMANI NILIPOHISI NILIKUWA KARIBU NA MUNGU!
SIKU HIZO NILIPOPITIA GIZANI, NILIFANYA HIVYO KAMA NIMEJAWA NA MWANGA WAKE!



VIJANA NA WAZEE WALINIHESHIMU NILIPOKETI NAO MJINI.
SIO KAMA NYINYI, WANA WA WAFALME NA WAKUU WANGESIKIZA NILIPOZUNGUMZA.
KWA NINI?
MAANAKE NILIBARIKIWA, NA NILIWABARIKI WALE WALIOKUWA NA MAHITAJI...
NILIWATETEA WALIOKANDAMIZWA...
NILIWALIWAZA WALIOKUWA WAMESONONEKA.
NILIWASAIDIA VIWETE, VIPOFU.
NILIKUWA KAMA MFALME!
SASA...
NACHUKULIWA VIBAYA ZAIDI YA MMOJA WA MBWA WANGU!




AYUB 29:7-30:1


MUNGU HANIBARIKI TENA.
NATAFUTA UZURI LAKINI NAPATA UOVU.
NATAFUTA MWANGAZA NAPATA GIZA.
NALILIA MSAADA HAKUNA ANAYEJIBU...
HAMNA ILA...NYINYI.
WAKATI MMOJA, SIO ZAMANI SANA, NILICHEZA KINANDA CHANGU NA WATU WALICHEZA NAMI!
SASA NAIMBA WIMBO WA HUZUNI KISHA MWATAFUTA KUHESABU DHAMBI ZANGU!
MAANAKE HICHO TU NDIO CHAWEZA KUELEZA...
HAPANA!!!
NIMEKUWA MUAMINIFU KWA MKE WANGU SIANGALII HATA MKE MWENGINE!
NASEMA KWELI WAKATI WOTE!
NIMEWASIAIDIA WANAOHITAJI MSAADA!
SIJAWAHI KUFURAHIKIA KUTESEKA KWA ADUI WANGU!






AYUB 31:1-32:22


WANUNG'UNIKA KUMHUSU MUNGU KUTOKUJIBU NA KUJIELEZA!
LAKINI MUNGU AZUNGUMZA, ILA SIO UNAVYOTARAJIA AU KUTAKA WEWE!
NDOTO... MANENO... MALAIKA...
NA MAPITIO... NA DESTURI... NA ADHABU...
ANAPOZUNGUMZA MUNGU, NI KUKUSAIDIA WEWE KUNJUA ZAIDI!
MUNGU ANAPOADHIBU, NI KUKUSAIDIA WEWE UGEUKE KWAKE!
SOTE TWASTAHILI MABAYA ZAIDI YA TUNAVYOPATA!
AFANYA ALIFANYALO KUTUTOA GIZANI NA KUTUELEKEZA KWENYE MWANGAZA!
ELIHU, SINA HATIA, ILA MUNGU ANINYIMA NAFASI YA KUZUNGUMZA! KISHA HANIJIBU NINAPOULIZA!
HAKUNYIMI CHOCHOTE!
KAMA MUNGU HASKIZI MAOMBI YA UONGO--
--KAMA HAWAZUNGUMZII WASEMAO KWA KIBURI--
--MBONA AJIBU SASA KWA SABABU TU UMECHOKA KUSUBIRI?


MUNGU HAWATESI WATU!
NI MWALIMU, NA MWALIMU KWELI, MAANAKE SHERIA AIFUNZAYO NI SHERIA ALIYOIUMBA!
ULIMWENGU WENYEWE UNA WAJIB KWAKE YEYE!
RADI YENYEWE HAILINGANI NA SAUTI YAKE!
AZIAMBIA MVUA NA THELUJI ZITAKAPOANGUKA!
UPEPO HAULINGANI NA PUMZI YAKE!
NA WASEMA YU KIMYA?
YUKO HAPA AYUB!
YWAZUNGUMZA!
MIMI NI MPUMPAVU NIKILINGANISHWA NA WENGINE, LAKINI SIO MJINGA WA KUTOSHA KUONGEA ULIVYOFANYA.
MUNGU YU MWENYE NGUVU KUU, HAKI NA UTAKATIFU.
NI SAWA KUMUOGOPA!
NI SAWA KUINAMA MBELE YA ANAYEAMRISHA DHORUBA AINA HII!
NDIO...


NDIO...
NDIO, NI SAWA.


AYUB...
NDIO BWANA?
AYUB...
WAZUNGUMZA KANA KWAMBA WAELEWA KILA KITU!
ILA MANENO YAKO YAKOSA HEKIMA YANGU!
NILIKUWA NAJIBU UJINGA WAO...
AYUB!!!
NAZUNGUMZA NAWE!
SIO WAO!
NDIO BWANA.



AYUB 38:1-2


SASA NINA MASWALI NATAKA KUKUULIZA NA NATAKA UYAJIBU!
NDIO, BWANA.
NITA... NITAJARIBU
NILIPOBUNI ARDHI NA KUIFINIKA NA MAWINGU NA KUZIFANYA NYOTA ZIIMBE NA MWANGAZA- -
- - ULIKUWAPO?
WAWEZA KUELEZA ILIVYOFANYIKA?
USHAWAHI KUTENGENEZA DUNIA KUTOKA KWA UDONGO NA KUGAWA MWANGA KUTOKA KWA GIZA?
UMEZIINGIA CHEMCHEMI ZA BAHARI?
WAWEZA KUFANYA NYOTA ZICHEZE ULIMWENGUNI?



JE, NI KWA MKONO WAKO SIMBA WACHANGA WALISHWA?
WATAZAMA PAA ANAPOZAA?
WASIKIA MLIO WA NDEGE WANAPOTOKA KWENYE YAI?
WAMPA FARASI NGUVU ZAKE KUU?
WAJUA ANAVYOPAA MWEWE?
KWA HIVYO NIJIBU, AYUB! UTANIAMBIA VILE MAMBO YANAVYOFAA KUFANYWA?
SI... SINA JIBU.
BASI JIBU MASWALI HAYA!




AYUB 40:15-40:24


MAMBA!
JARIBU KUMSHIKA KWA NDOANA!
WAWEZA KUMSHIKA NA KUMFANYA AKUNONGONEZEE KAMA AMBAYE U BWANA WAKE?
NGOZI KAMA SILAHA! KIFUA KAMA JIWE!

AYUB 41:1-34


NILIWAUMBA VIUMBE HAWA NA HAKUNA ANAYEWEZA KUSIMAMA DHIDI YAO!
NANI, BASI, AWEZA KUSIMAMA DHIDI YANGU?
AYUB NILIUUMBA ULIMWENGU. NIKAIKAIFINYANGA ARDHI.
NIKAIJAZA NA VIUMBE VIKUU NA VIDOGO
NIKAKUUMBA WEWE.
NIAMINI.
AYUB 38-41


NAJUA WAWEZA KUVIFANYA VITU VYOTE.
NAJUA UNA MIPANGO INAYOZIDI MAWAZO NA NGUVU ZA BINADAMU.
ULIULIZA ALIYE NA HEKIMA YAKO, NGUVU ZAKO, NA UTAKATIFU WAKO.
NANI ALIYEKUWA NA SHAUKU JUU YAKO BILA HATA KUIPATA PICHA KAMILI?


MIMI.
NISAMEHE.



AYUB 42:1-3


SINA MAJIBU KWA MASWALI ULIYOYAULIZA, WEWE TU NDIYE UJUAYE MAJIBU HAYO.
MPAKA SASA NAISHI NIKISTAAJABISHWA NAWE KUTOKANA NA NILICHOKISIKIA.
ILA SASA NIMEKUONA KWA MACHO YANGU NA KUKUSIKIA KWA MASIKIO YANGU...
NISAMEHE!
SINA HEKIMA YAKO, LAKINI NINA IMANI NA HEKIMA YAKO!
MACHO YANGU YALITAZAMA NDANI, KWANGU MIMI; NAYAGEUZA MACHO YANGU NJE, KWAKO WEWE!
SINA HASIRA NAWE, AYUB.
ULIKUWA NA MASWALI KWANGU NA JUU YANGU, LAKINI HUKUZUNGUMZA DHIDI YANGU.
NAKUITA MTUMISHI WANGU; NAKUITA RAFIKI YANGU.
NYINYI WATATU...


INGAWA NIMEZUNGUMZA NA AYUB KUMREKEBISHA SIO KWA SABABU AMENIKASIRISHA.
INGAWA NYINYI MUMENIKASIRISHA.
MLIZUNGUMZIA NGUVU ZANGU NA HAKI MKAPUUZA MAMLAKA YANGU NA REHEMA!
MLIMUITA AYUB MUINGO, MNAFIKI, MWENYE DHAMBI! MKASEMA NAMUADHIBU!
HAMJAZUNGUMZA JUU YANGU KWA HAKI, ALIVYOFANYA AYUB.
KILA MMOJA WENU ATOE NG'OMBE DUME WASABA NA KONDOO DUME WASABA KAMA KAFARA ILIYOCHOMWA KWANGU.
NITAKUBALI OMBI LA AYUB KWA NIABA YENU NA SITAWAPA MNACHOKISTAHILI.
TUBU.


HUU...HUU WAKATI WA KUOMBOLEZA UMEISHA.
NA...NADHANI NI WAKATI WA KURUDI NYUMBANI.
AYUB, UKO SAWA?
NDIO... NA LA...
BADO NAHISI UCHUNGU, NAUMIA KWA SABABU YA WANANGU...
AYUB?
KAMA MWAPANGA KUKIFANYA MUNGU ALICHOWAAMBIA, NITAWANGOJEA KWANGU NYUMBANI.

AYUB 42:9


NJOO AYUB, NITAKUSAIDIA KUFIKA NYUMBANI
AYUB?
NINI KINAFANYIKA?
SI... SIJUI.
JAMBO MOJA TU SI...SIELEWI!
NA KITU KIMOJA TENA CHA KUMSHUKURU MUNGU!




MARAFIKI WA AYUB WALIFANYA WALIVYOAMBIWA NA MUNGU.
NA AYUB PIA, ALIFANYA ALIVYOAMBIWA NA MUNGU.
BWANA, MARAFIKI ZANGU WAJA KWAKO NA KAFARA HII!
WANATAMBUA NA KUTUBU DHAMBI ZAO!
WANATOA KAFARA HII KAMA MALIPO KWA DHAMBI ZAO DHIDI YAKO!
NA BWANA ALIFANYA ALIVYOAHIDI.

AYUB 42:9


UTAWAHI KUJUA KWA NINI YOTE YALITENDEKA?
ILIKUWA KUKUPA FUNZO AYUB?
KUTUPA SISI FUNZO?
AU WALE WATAOKUJA BAADA YETU?
LABDA HAYO YOTE...
...AU MENGI ZAIDI YA KUELEWA KWETU!
WAKATI HUO WOTE, ULIULIZA MTU ASIMAME KWA NIABA YAKO MBELE YA MUNGU.
NA SASA, BAADA YA SISI KUKUFELI, WASIMAMA KWA NIABA YETU!
BARAKA ZA MUNGU ZIWEPO JUU YAKO RAFIKI YANGU.
NIMEHESHIMIKA KUWA WEWE NI RAFIKI YANGU.
ITAKUWAJE HAUTUCHUKII BAADA YA TULIVYOKUZUNGUMZIA?
KWA SABABU MUNGU HATUCHUKII HATA BAADA YA KUTENDA TUNAVYOMTENDEA!

AYUB 42:9


ELIHU ASANTE KWA KUWA NGUZO YANGU.
NA NAKUSHUKURU KWA KUBAKIA RAFIKI YETU.
NILIDHANI NIMEKUPOTEZA, WAJUA.
NILIKUWA NA UHAKIKA MUNGU AKUCHUKUA KUTOKA KWANGU PIA.
NILITAKA ANICHUKUE... MPAKA ALIPOZUNGUMZA NAMI.
NATAMANI TU ANGEKUPA JIBU!
ALINIPA!
LAKINI ULISEMA HAKUKUAMBIA NI KWA NINI!
HAKUNIPA JIBU NILILOLITAKA, LAKINI ALINIPA JIBU BILA SHAKA.



AYUB 42:10


SINA UHAKIKA TUNGEWEZA HATA KUELEWA KAMA TUNGEJUA SABABU.
LAKINI SISHUKU NGUVU ZA MUNGU, UTAKATIFU WAKE, NA MAPENZI YAKE KWETU.


MUNGU ALIYABARIKI MAISHA YA AYUB ZAIDI YA AWALI.
KARIBUNI ALIKUWA NA MIFUGO KULIKO HAPO AWALI, NA WANA KUMI ZAIDI.


NA VIZAZI VYA WATOTO.
NA AKAFA MZEE NA WINGI WA MIAKA.

AYUB 42:11-17





SUPERBIBLE.TV